# UUMBAJI WAKE WA PILI

*2 Wakorintho 5:17 . Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! Yamekuwa mapya.*
*Ufunuo 3:14. Na kwa malaika wa kanisa lililoko laodikia andika; haya ndiyo anenavyo yeye aliye Amina. Shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu.*

Hebu na tuone kile Nabii wa Mungu wa siku hii alivyosema juu ya hilo;

"Mwanzo wa kuumba kwa Mungu." Huyo ndiye ambaye Bwana Yesu anayasema ya kwamba ni yeye Mwenyewe. Lakini maneno hayo hayamaanishi jinsi hasa kama yanavyosikika kwetu. Kuyachukua tu jinsi yanavyosikika yamewafanya baadhi ya watu Fulani (kusema kweli ni umati wa watu) kupata wazo kwamba Yesu alikuwa kiumbe cha kwanza kuumbwa na Mungu. Likimfanya yeye kuwa mdogo kuliko Mungu. Ndipo kiumbe hiki cha kwanza kikaumba ulimwengu wote mwingine na chochote kilichomo ndani yake. Lakini hiyo si kweli. Unajua jambo hilo haliambatani na sehemu iliyosalia ya biblia. Maneno hayo ni, "yeye ndiye MWANZO ama MWANZILISHI wa kuumba kwa Mungu." Sasa tunajua kwa hakika ya kwamba Yesu ni Mungu, Mungu halisi. Yeye ndiye Muumbaji. Yohana 1:3 "Vyote vilifanyika kwa Huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika." Yeye ndiye ambaye alinenwa, mwanzo. 1:1 "Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi." Pia inasema katika
Kut, 20:11, "Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba." Unaona, hapana shaka ya kwamba yeye ndiye muumba. Alikuwa Muumba wa UUMBAJI WA MAUMBILE YALIYOMALIZIKA.

Hakika tunaweza kuona kile ambacho maneno haya yanamaanisha sasa. Kuwa na tafsiri nyingine yoyote ingemaanisha ya kwamba Mungu alimuumba Mungu. Mungu angewezaje kuumbwa wakati yeye, Mwenyewe, ndiye Muumba?

Lakini sasa yeye anasimama katikati ya kanisa. Wakati anaposimama pale akijifunua yeye yu nani katika wakati huu wa mwisho, yeye anajiita "Mwanzo wa kuumba kwa Mungu ." huu ni UUMBAJI MWINGINE. Hili linahusiana na kanisa. Hii ni sifa nyingine maalum yake mwenyewe. Yeye ndiye MUUMBA wa kanisa hilo. Bwana arusi wa mbinguni alimuumba bibi – arusi wake. Akiwa Roho wa Mungu, alishuka na kuumba katika bikira Mariamu chembechembe zenyewe katika tumbo la uzazi la Mariamu kwa ajili ya mwili huo. Haikutosha kwa Roho Mtakatifu kutia uhai kwa urahisi tu katika yai la mwanadamu lililotolewa na Mariamu. Hiyo ingekuwa ni mwanadamu mwenye dhambi akiuzaa mwili. Hilo halingeweza kumzaa "Adamu wa Mwisho." Kumhusu Yesu ilisemwa "Tazama mwili wewe (Baba) umeniweka tayari."Mungu (si Mariamu) ndiye aliyetoa mwili huo. Mariamu alikuwa chombo cha kibinadamu cha kuangalia naye alimbeba mtoto Mtakatifu na akamzaa. Alikuwa Mungu-mwanadamu. Alikuwa ni Mwana wa Mungu. Alikuwa ni wa ule uumbaji MPYA mwanadamu na Mungu walikutana na kuungana; yeye alikuwa ni wa kwanza wa jamii hii mpya. Yeye ndiye kiongozi wa jamii hii mpya. Kol 1:18, "Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; Naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote." 2Kor 5:17 "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! Yote yamekuwa mapya." Hapo unaweza kuona ya kwamba ingawa mwanadamu alikuwa ni wa UTARATIBU ule WA KALE ama uumbaji, sasa katika KUUNGANA NA KRISTO YESU tutende matendo mema." Efe 4:24, "mkavae UTU MPYA ulioumbwa kw namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli." Huu Uumbaji mpya si ule uumbaji wa kale uliotengenezwa tena, la sivyo haungeitwa uumbaji mpya. Hivi ndivyo hasa inavyosema ulivyo, UUMBAJI MPYA."Ni uumbaji mwingine, mbali na ule wa zamani. Hashughuliki tena na mambo ya mwili. Hivyo ndivyo alivyoshughulika na Israeli. Alimchagua Ibrahimu, na uzao wa Ibrahimu kw akupitia ukoo mcha Mungu wa Isaka. Lakini sasa kutoka katika kila jamaa, kanila na taifa yeye amekusudia kiumbe kipya. Yeye ndiye wa kwanza wa uumbaji huo. Yye alikuwa ni Mungu aliyeumbwa kwa mfano wa mwnadamu. Sasa kwa Roho wake yeye

anajiumbia wana wengi mwenyewe. Mungu muumba, akijiumbia Mwenyewe sehemu ya uumbaji wake. Huu ndio ufunuo wa kweli wa Mungu. Hili lilikuwa ndilo kusudi lake. Kusudi hili lilifanywa halisi kwa uchaguzi. Hiyo ndiyo sababu yeye aliweza kkuangalia oja kwa moja hata kwenye wakati wa mwisho wakati yote yatakuwa yamekwisha na kujiona Mwenyewe angali akiwa katikati ya kanisa, kama mwanzilishi wa huu Uumbaji Mpya wa Mungu. Nguvu za ukuu wake zilitimiza jambo hilo. Kwa amri yake Mwenyewe yeye aliwachagua washiriki wa uumbaji huu mpya. Aliwachagua tangu zamani wapate kufanywa wana kulingana na uradhi wa mapenzi yake. Kwa kujua kwake yote na kwa kuwa kwake na nguvu zote alilitimiza. Vinginevyo angwezaje kujua kwamba angesimama katikati ya kanisa akipokea utukufu kutoka kwa ndugu zake kama yeye hakuhakikisha? Alijua mambo yote, na alitenda mambo yote kulingana na yale aliyoyajua ili kwamba kusudi lake na uradhi wa mapenzi yake vitimizwe. Efe 2:11 "Ndani yake isi nasi tulifanywa wraith, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake." Haleluya! Je! Hufurahi ya kwamba wewe ni wake! [1]

Nimewaona washutumu wakisimama pembeni na kuunenea vibaya, na hufanya yasiyofaa kwenye uamsho wa Roho Mtakatifu na baada ya muda Mungu anamwingia mtu huyu huyu na kumgeuza, na anasimama hapa mimbarani na kuhubiria kitu kile kile ambacho mwanzoni alikichukia. Ni kitendawili, jinsi Mungu anayomchukuwa asiyeamini na kumfanya kuwa mwaminio.

Hakuna hata mmoja awezaye kulielezea hilo. Lakini ni kitendawili, kwa sababu ni muujiza wa Mungu. Mtu anapobadilishwa kutoka utu wake alio nao kuwa kiumbe kipya ndani ya Yesu kristo, anakuwa uumbaji mpya. Hayuko tena vile alivyozoea kuwa ( Wagalatia 6:15-16 ). Amekuwa hakika uumbaji mpya ndani ya kristo [2]

Kama huna chochote kinachoweza kulifanya kanisa litembee kwa usahihi, lifanye kwa usahihi lijionyeshe lenyewe, ni ubatizo wa Roho Mtakatifu na moto (Matayo 3:7-12) ukishuka chini kutoka mbinguni kwa Mungu utalinyoosha kanisa hasa, siyo kuzoza juu ya hili au juu ya kile, lakini ni ubatizo wa moto wa upendo wa Mungu ambao unashuka chini na kusafisha vitu vitoke katika moyo wako (Warumi 5:3-5), inakufanya wewe kiumbe kipya ndani ya Kristo Yesu. Wanawake wataacha nywele zao zikue na wanaume wataacha kuvuta sigara na ninakuambia….Na mambo haya mengine yatanyooshwa kama utauleta tu ule moto uwe juu yao. Kweli [3]

Wakati Mungu alipomuumba mtu wa kwanza, akaumba mbingu na nchi, na Mungu aliposimama nyuma juu ya uumbaji ule wa zamani na kuuangalia ulivyokuwa, Hakuuangalia ili auhukumu huo. Aliuangalia, na kusema, "Tazama jinsi ulivyo ni mzuri sana" aliupenda huo oh, jamani unaona hilo? Aliuangalia na kuona jinsi ulivyo kuwa mzuri. Kila kitu kilikuwa kikamilifu. Alisema "Tazama kila kitu ni chema sana" (Mwanzo 1:31) lakini sasa, shetani aliupotosha huo.

Lakini kama Mungu hakuweza kuulaani uumbaji wake wa kwanza, ni jambo lisilowezekana zaidi sana kwa yeye kuulaani uumbaji wake wa pili, wakati umeumbwa kiumbe kipya ndani ya Yesu Kristo (Waefeso 2:14-17). Huwezi ukalifanya hilo wewe mwenyewe. Haijalishi unataka kwa kiasi gani, huwezi ukalifanya hilo. Ni kipawa cha Mungu "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu asipovutwa na baba (Yohana 6:44). Na wote wanaokuja kwangu, nitawapa uzima wa milele na kuwafufua siku ya mwisho. (Yohana 6:39-40).

Na wakati Mungu amekuzaa wewe upya kwa Roho Mtakatifu, Anaweza akakuangalia wewe tu kama kazi ilivyo kamilifu, kwa sababu ameitenda yeye mwenyewe (Yohana 3:1-8) utukufu Amen Amen. Hawezi akahukumia wewe hatia, kwa sababu u kazi yake mwenyewe (Waefeso 2:10) Amen oh jamani najisikia kupiga makelele kama mmethodist fikiria hilo wewe u kazi yake Mungu mwenyewe. Aliifanyaje hiyo? Kwa neema yake isiyo na mipaka siyo kwa sababu mliruka, siyo kwa sababu ulienda kanisani, siyo kwa sababu ulifungua ukurasa mpya, Lakini kwa sababu ya huruma zake Mungu, amekuleta wewe ndani ya Kristo na kuwa na ushirika, na kukuangalia wewe kama kazi yake mwenyewe iliyokamilifu kwa nini? "Nimemnunua yeye; Nikamwakilisha katika damu na pale hakuna ambacho siyo sahihi kwa kazi yangu," Alisema ninyi kazi yake Mungu mwenyewe [4].

Ameanzisha uumbaji mpya ilikuwa ni nini? Uumbaji wake mwenyewe Mungu alifanyika mwili na akakaa kati yetu (Yohana 1:14) Biblia

ilisema, "pale mwanzo wa uumbaji wa Mungu Mungu aliumbwa katika mfano wa Mwanadamu; ndani ya Yesu Kristo, mwana wake, Mungu alikaa. Alijenga maskani/makao yake ya mwili na mifupa, na akaishi katika nyumba hiyo. Mungu, Immanuel,"Mungu pamoja nasi" (matayo 1:21-23) alijenga nyumba yake mwenyewe na kukaa ndani yake, ili aweze kulidhihirisha neno lake kwa walio wake kupitia huyo. Unamjua Mungu alivyo unapomuona Kristo [5]

Kabla ya kuwekwa misingi ya dunia jina lake liliwekwa katika kitabu cha uzima cha mwana kondoo halafu kutoka hapo akawa Neno, ile theophery mwili uwezao kuonekana na kutoweka; na halafu akafanyika mwili na akarudi tena, akaufufua mwili ule ule katika hali iliyotukuzwa lakini wewe uliruka ule mwili wa theopary na ukafanyika mwili mtu wa kujaribiwa na dhambi. Na baadaye "Kama nyumba hii ya maskani yetu hii ya dunia ikiharibiwa, tunao mwili ulio tayari unatungojea" (2 kor 5:1) Bado hatunayo miili hiyo lakini angalia wakati miili hii inapopokea Roho ya Mungu, ule uzima wa milele ulio ndani yako, unauweka mwili huu katika hali kumtii/ kutawaliwa na Mungu (Rum 8:11) Halleluyah.

"Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; hawezi kutenda dhambi" (1Yohana 3:9).

Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu; Hawaenendi kwa kuufuata mwili, bali kwa kufuata Roho (Rum 8:1). Hilo hapo unaona, hiyo inaufanya mwili wako utiishwe huna haja ya kusema, "oh, kama tu ningeweza kuacha kulewa, kama tu ningeingia tu ndani ndani ya Kristo; yote hayo yanaondoka kwa sababu mwili wako unatiishwa na Roho, hautiishwi tena na mambo ya dunia; yamekufa yamekufa dhambi zako zimezikwa katika ubatizo (Rum 6:3-4); na wewe ni uumbaji mpya ndani ya Kristo na mwili wako unakuwa unaotiishwa na Roho, ukijaribu kuishi maisha sahihi….

Kama ninyi wanawake mnaodai kuwa mna Roho Mtakatifu na mnatoka nje kule na kuvaa kaptura na mengineyo, utafanyaje hivyo? Yawezekanaje Roho wa Mungu ndani yako akuache utende jambo kama hilo? Haiwezekani iwe hivyo. Hakika haiwezekani iwe hivyo yeye siyo Roho mchafu; yeye ni Roho Mtakatifu.

Na unapotiishwa kwa Roho huyo inautupa utu wako wote utiishwe na yule roho. Na huyo Roho siyo chochote kile duniani ila ni hii mbegu ya Neno inapodhihirishwa au ikihuishwa (Haleluyah) inafanywa hai. Na Biblia inaposema, "Usifanye hivi" ule mwili haraka unageuka; hakuna swali na ni nini? Ni arabuni ya ufufuo (Efeso 1:13-14, 2 Kor 1:21-22) Huu mwili utafufuliwa tena, kwa sababu umeshaanza tayari. Kwnza uliitishwa katika dhambi na uchafu na uharibifu, lakini sasa unayo arabuni; umegeuka wa kimbinguni (Warumi 6:15-19). Sasa hiyo ni arabuni ya kuwa unaenda kunyakuliwa ni arabuni

Mtu mgojwa amelala anakufa, hakuna kilichobakia ila kifo, hilo ndilo tu liwezalo kutokea. Nimeona vivuli vya watu walioliwa na saratani (Kansa) na kifua kikuu, na kuwaona tena watu hao baadaye wakiwa na hali kamilifu na wenye nguvu kama hakuna uponyaji wa kiungu basi sasa hakuna ufufuo kwa sababu uponyaji wa kiungu ni arabuni ya ufufuo Amen.

Unajua nini arabuni ya pesa ni nini? Ni kiwango cha chini unacholipia kitu kwamba utakichukua. "Aliyejeruhiwa kwa makosa yetu; na kwa kupigwa kwake sisi tumepona" (1Petro 2:21-25) [6]

Huko tena vile ulivyokuwa wewe ni kiumbe kipya kwa maana kile kiyunani kunamaanisha "Uumbaji mpya" Umeumbwa upya tena Nguvu za Mungu zinakuja juu yako na unakuwa aliyeumbwa tena, kiumbe kipya (Tito 3:4-7) ambayo inaleta utu wote wa mwili utu wa Rohoni na kila kitu, viwe vitiifu kwa Neno la Mungu, siyo hapana njia nyingine wawezaje kusema wewe ni mkristo na usilitii Neno lake kwa kitu kimoja?

Hebu na tuwaangalie wale waliokuwa waaminifu pale Pentecoste. Wote walikuwa chumba cha juu pale, na wote walikuwa wanaogopa walikuwa na haki vizuri lakini walikuwa waoga. Na mara kwa ghafla ukaja uvumi toka mbinguni (ile ahadi ilishushwa chini) kama uvumi wa upepo wa nguvu uendao kasi, ukaijaza nyumba yote waliyo kuwa wameketi (Matendo 2:1-13) na wakahuishwa sana na huo, mpaka woga wao wote waliokuwa nao…Mmoja wao alikuwa mwoga mpaka akakana kwamba yeye hajawa Farisayo bado, au hajawa sedukayo bado. Lakini Roho Mtakatifu aliposhuka na kumbatiza yeye ndani ya Yesu Kristo (1kor 12:13) akawa nyama ya nyama yake mfupa wa

mfalme wake Neno la Neno lake (waefe 5:30-32) Alikuwa ni kiumbe kipya. Alikuwa ni mtu mpya ilihuisha mwili wake [7]

Hapo ni uumbaji mpya, siyo kwa dhehebu, ila kwa Neno. Umekuwa uumbaji wa Neno. Kwa sababu jiwe la msingi liliwekwa ndani yako kabla ya kuwekwa misingi ya dunia ulikusudiwa kuwa mwana na binti wa Mungu. [8]

Kamwe hutamfahamu Kristo kwa theolojia kamwe hutamfahamu Kristo kwa Elimu itakupasa umfahamu Kristo kwa uzoefu wako binafsi kwa kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wake ambaye anakuja chini na kubadilisha maisha yako na kukufanya wewe kiumbe kipya ndani ya Kristo Yesu; hicho ndicho kinacholeta tofauti. Hicho ndicho kinachokufanya wewe uwe tofauti sasa, hiyo ndiyo sababu tuna madhehebu mengi tofauti na kanunu mbalimbali [9]

Ukristo siyo uigizaji. Ni maisha ukristo unakuja kwa kuzaliwa kwamba umezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu na unakuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo Yesu. Mambo ya kale yamepita na mambo yote yanakuwa mapya Angalia [10]

Ngoja nikuambie; usijiunge tu na kanisa sasa. Hilo halitafanya kazi unapaswa uzaliwe mara ya pili; siyo msisimko wa kujiumbia, sio jambo Fulani ulilosema, "Vema nilipiga makelele. Nilinena kwa lugha nimefanya hiki na kile au kinginecho". Wakati moyoni mwko hasa, kitu Fulani kinakuja na kukubadilisha wewe, na unakuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo Yesu, unampokea yule mtu, Kristo Yesu wakati mambo ya kale yanapokufa, na mambo mapya yanazaliwa tena, unasahihisha mambo yasiyo sawa ambayo uliyafanya; unawapenda maaadui zako; unawaombea wale wanokuudhi. Hapo ndiyo sasa ni mkristo (matayo 5:43-48) Mti unajulikana kwa matunda unayozaa (Matayo 7:15-20) [11]

Oh, usidanganyike halafu shetani ananjia nyingine. Tuna muda mfupi uliobaki kwa hili. Shetani anayo njia nyingine ya kupotosha, mbali na kusema….unasema, "vema siigwi ndugu Brahamu sivuti. Sipigi kamari . Sitembei nje ya Mume wangu, au mke wangu. Ninaishi maisha mazuri "lakini shetani amepotosha hayo. Anakuacha wewe ufikiri kuridhisha dhamira yako yenye hatia, kumbe unaenda unajiunga na kanisa, na wewe uko sahihi. Hiyo ni makosa huo ni upotoshaji.

Huwezi ukapata utoshelezi kwa kujiunga na kanisa. Unakuwa tu wa wa kiakili. Ni jambo la kielimu. Lakini kamwe hutaweza kutosheka mpaka umjue yeye, kama anayesamehe dhambi zako zote, ambapo swala la dhambi limemalizwa, na unao ule upendo, amani, utulivu, uzima, ushirika wa milele pamoja naye wakati amani ya Mungu inayopita ufahamu wote imekutakasa nafsi yako, na kukufanya wewe kuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo Yesu (Wafilipi 4:6-7) [12].

Na hiyo ni kweli marafiki, utajiri haupimwi kwa kutumia dola utajiri haupimwi kwa majina makubwa na kuwa maarufu. Utajiri ni wakati ufalme wa Mungu umekuja ndani ya mioyo ya wanadamu, imebadilisha shauku zake na kumfanya yeye kuwa kiumbe kipya ndni ya Kristo Yesu, na kumpa yeye uzima wa Milele (yohana 5:24)
Huo ndio utajiri mkuu sana duniani.

Wewe ni maskini katika vitu vya dunia hii? Hujui hata vile utakavyolipa bili ya mkaa au bili ya mafuta au chochote kile? Unaweza ukawa hivyo; Natumaini huko hivyo. Lakini kama uko hivyo, unaweza ukaondoka kwenye jengo hili usiku wa leo ukiwa maskini mwenye furaha duniani humu. Unaweza ukaondoka hapa usiku wa leo na utajiri ambao dunia haiwezi kununua. Unaweza ukaunganisha moyo wako na Kristo Yesu na anaweza akaja ndani ya nafsi yako na kuchukua uongozi katika chumba cha kuongozea. Na haijalishi kuna kuja nini au kunatokea nini, utakuwa na furaha maisha yako yote yaliyobakia [13].

Usitegemee utaratibu wa aina yoyote, au msisimko wa aina yoyote, au hiki na kile. Kutana na Mungu na Mungu peke. Ufikie pale mpaka maisha yako yamebadilishwa na unakuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo. Mungu atashughulika na sehemu nyingineyo yote kama anataka wewe ufanye kitu chochote, unaweza ukazungumza naye. Naye atakuambia wewe [14]

**Nukuu za Kiingereza**
[1] Wakati wa loadikia" Kitabu cha nyakati za kanisa uk 336 - 337
[2] Kitendawili (63 – 0801) Aya 32/

[3] Sauti zisizo na uhakika (61-0315)
[4] Ushirika ni kwa ukombozi, Aya 215 – 217 /
[5]kwa nini ilikuwa ni wachungaji Aya 98
[6] Huyu malkizedeki ni nani Aya 70-75
[7] Mahali Mungu alipopachagua pakuabudia (65-0425) Aya 97-161
[8] Mahali pekee Bwana alipopachagua pa kuabudia (65-1128M) Aya 251
[9] Kuishindania Imani (56-0421E) Aya 17
[10] Mungu aliweka ahadi zake ( 56-1209A) Aya 251
[11] Macho yao yakafunguka (57-0421E )Aya 8
[12] Uhai (57-0602) Aya 41
[13] Umoja wa Mungu katika kanisa moja (58-1221E) Aya 142
[14 ] Dunia inaanguka na inazunguka (63 – 0412M), Aya 51

Jiwe la kiroho la kujengea na. 158 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*